USAJILI WA WADAU WA TASNIA YA NYAMA

1. UTANGULIZI

Tasnia ya nyama hapa nchini inasimamiwa na Sheria ya Nyama Na. 10 ya Mwaka 2006. Sheria hii ilitungwa kutokana na kuwepo kwa ombwe katika usimamizi wa tasnia ya nyama baada ya kuvunjwa kwa mamlaka ya kusimamia na kuendeleza mifugo na mazao yake (Livestock Development Authority - LIDA) mwanzoni mwa miaka ya 1980. Vile vile kumekuwepo na hitajio la nyama bora na salama katika soko la ndani na nje ya nchi.

Ili kusimamia utekelezaji wa sheria ya Nyama Na. 10 ya Mwaka 2006, Bodi ya Nyama Tanzania iliundwa chini ya kifungu 9 (1) kwa lengo la kuweka misingi thabiti ya kuendeleza uzalishaji, usindikaji, biashara ya mifugo, nyama na mazao yake inayozingatia ubora na viwango ili kukidhi mahitaji ya soko la ndani na nje ya nchi. Aidha, katika kutekeleza majukumu hayo Bodi haina budi kushirikiana na wadau mbalimbali zikiwemo Mamlaka za Serikali za Mitaa, hivyo Bodi imeandaa kanuni na miongozo ya ukaguzi, upangaji wa madaraja ya mifugo na nyama na usajili wa wadau wa tasnia ya nyama ili kuelekeza wadau katika kutekeleza majukumu yao kwa mujibu ya sheria. Ili kutekeleza usajili ni dhahiri kuwa ukaguzi ndio ufunguo wa utambuzi na usajili wa wadau wa Tasnia ya Nyama.

2.USAJILI WA WADAU WA TASNIA YA NYAMA

2.1 Lengo la Usajili

Kuwezesha wadau kushiriki kikamilifu katika kuendeleza tasnia ya nyama kuanzia kwenye uzalishaji, usindikaji, biashara ya mifugo, nyama na mazao yake. Vile vile inawezesha wadau kupatiwa huduma mbalimbali zikiwemo taarifa muhimu za tasnia na kuunda mtandao baina yao.

2.2 Wadau na Maeneo Yatakayosajiliwa

Watakaosajiliwa na kutambuliwa ni watu binafsi, taasisi, vyama vya kijamii kampuni na maeneo yanayotumika katika uzalishaji wa mifugo, Wadau wote wanaofanya shughuli za kibiashara katika hatua mbalimbali za mnyororo wa thamani wa nyama wakiwemo wadau waliosajiliwa na sheria nyingine kama Sheria ya Magonjwa ya Mifugo Na. 17 ya Mwaka 2003, Sheria ya Chakula, Dawa na Vipondozi Na. 1 ya Mwaka 2003, Sheria ya Maeneo ya Malisho na Vyakula vya Mifugo Na. 13 ya Mwaka 2010, Sheria ya Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji Na. 12 ya Mwaka 2010 watatambuliwa na kusajiliwa.

Wadau na maeneo hayo ni pamoja na:-

- Wafugaji wa mifugo wa nyama wa aina zote kwa ajili ya biashara;
- Wamiliki wa mashamba ya kati na makubwa (ranchi)
- Mfanyabiashara wa mifugo hai ndani na nje ya nchi
- Mfanyabiashara wa nyama (maduka ya Nyama) na mazao ya nyama
- Wakala wa biashara ya nyama na mazao ya nyama
- Vyama vya wadau vinavyotambulika kisheria;

- Minada ya mifugo
- Dalali wa Mifugo
- Mwendesha Minada
- Wamiliki wa Minada/Masoko ya mifugo
- Watengenezaji/ Waagizaji / Wasambazaji wa mashine za uzalishaji wa nyama na pembejeo za nyama
- Machinjio na Viwanda vya Nyama na bidhaa za Nyama
- Waendesha matamasha ya Nyama na Wakala wa biashara ya nyama na bidhaa za nyama
- Waingizaji na wauzaji wa nyama ndani na nje ya nchi.

3. VIGEZO VYA USAJILI

3.1 Mfugaji/Mmiliki wa shamba dogo la mifugo

- Awe na eneo la ufugaji linalotambuliwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa na awe na anuani ya kudumu.
- Awe amesajili shamba na mifugo kwa mujibu wa Sheria ya Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji na kutunza kumbukumbu zake kwa ajili ya ufuatiliaji.
- Awe mfugaji anayefuga kwa lengo la biashara.
- Awe analisha mifugo yake vyakula vinavyotambuliwa na Sheria za Magonjwa ya Wanyama Na. 17 ya mwaka 2003 na Maeneo ya Malisho na Vyakula vya Mifugo Na. 13 ya mwaka 2010.
- Awe anamilki mifugo ya nyama isiyopungua ng'ombe 5 hadi 49 au mbuzi 20 hadi 299 au kondoo 20 hadi 299 au nguruwe 15 hadi 99 au kuku 400 hadi 999 kwa wakati mmoja kwa mwaka.

Mashamba ya kati na makubwa/Ranchi

- Liwe eneo la ardhi linalotambulika na kumilikiwa kisheria, liwe na anuani;
- Liwe na uwezo wa kuweka mifugo isiyopungua ng'ombe 50 au mbuzi 300 au kondoo 300 au nguruwe 100 au kuku 1,000 kwa mwaka; na
- Shamba na mifugo liwe limesajiliwa kwa mujibu wa Sheria ya Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji na kutunza kumbukumbu zake kwa ajili ya ufuatiliaji.

3.2 Minada ya Mifugo

- Mnada wa awali, upili au mpakani ulioanzishwa kisheria
- Mnada unaokidhi mahitaji ya miundombinu ikiwemo mizani, eneo la kupumzisha mifugo, kiringe cha kunadishia kama ilivyoelekezwa kwenye Kanuni Na. 6 ya kuanzisha, kusimamia na kuendesha minada ya mwaka 2010.

3.3 Msimamizi wa Mnada

- Awe mwenye elimu ya kiwango kisichopungua Astashahada ya uzalishaji na afya ya mifugo kwa minada ya awali na Stashahada ya uzalishaji wa mifugo kwa minada ya upili na mipakani
- Awe ameteuliwa na mamlaka husika.

3.4 Dalali

- Awe na leseni ya udalali
- Awe ameomba kazi ya udalali katika mamlaka husika inayomiliki mnada na kukubalika
- Awe na uzoefu wa biashara ya mifugo.

3.5 Mfanyabiashara wa Mifugo hai ndani na nje ya nchi

- Awe na anuani
- Awe analipa kodi za serikali
- Awe na leseni ya biashara.

3.6 Mfanyabiashara wa Jumla na rejareja wa mifugo na nyama ndani na nje ya nchi

- Awe na anuani pamoja na leseni ya biashara;
- Awe analipa kodi za serikali
- Awe na eneo la biashara linalokidhi viwango; na
- Awe na kibali cha TFDA

3.7 Vyama na Vikundi vya Wadau

Vyama vitakavyosajiliwa ni pamoja na vyama na vikundi vya wafugaji, wafanyabiashara, wasindikaji, walaji, wauza pembejeo, wauzaji na waangizaji nyama, bidhaa zake na pembejeo nje ya nchi.

Vyama hivyo vinatakiwa kuwa na sifa zifuatavyo:-

- Viwe vimesajiliwa kisheria
- Viwe na Katiba
- Viwe na ofisi yenye watendaji na inayofanya kazi
- Viwe na vyanzo/njia mbalimbali za kuongeza mapato na akaunti benki
- Viwe na wanachama hai
- Viwe hai na vinavyofanya mikutano kwa mujibu wa katiba.

3.8 Wadau wengine watakaotambuliwa

Wadau wengine na maeneo yao ambao vigezo vyao havikufafanuliwa watasajiliwa kulingana na Sheria za Magonjwa ya Mifugo, Chakula, Dawa na Vipondozi, Maeneo ya Malisho na Vyakula vya Mifugo na Sheria ya Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji. Bodi ya Nyama itasajili wadau hao kwa lengo la kutambuliwa na kuratibu shughuli zao katika kuendeleza zao la nyama. Ni pamoja na:-

- Machinjio
- Wasindikaji
- Wasambazaji wa nyama na mazao yake na
- Waagizaji na wauzaji wa nyama na mazao ya nyama nje ya nchi

4. UTARATIBU WA KUSAJILI

Utaratibu wa kusajili wa wadau na maeneo ya uzalishaji mifugo utazingatia mambo yafuatayo:-

- Mwombaji mwenye sifa ataomba usajili kwa kujaza fomu maalum zinazopatikana katika ofisi zote za Mifugo zilizopo katika Mamlaka za Serikali za Mitaa na Ofisi ya Msajili wa Bodi ya Nyama Tanzania kwa gharama ya shilingi 2,000/-ambazo hazitarejeshwa.
- Mwombaji atajaza fomu hizo na kuzirudisha kwenye ofisi ya Msajili Msaidizi wa eneo husika.
- Msajili Msaidizi wa eneo husika atakagua eneo na nyaraka muhimu na kujaza mapendekezo yake kwenye kwenye fomu ya mwombaji.
- Mwombaji atalipa ada ya usajili kulingana na shughuli zake anazoombea usajili.
- Fomu hizo zitatumwa kwa Msajili wa Bodi ambaye atazihakiki kabla ya kuziwasilisha kwenye Kikao cha Bodi kwa maamuzi ya usajili.
- Bodi itaidhinisha au kukataa usajili wa mwombaji endapo atakidhi au hatakidhi vigezo vya usajili.
- Mwombaji atakayepata usajili atapewa cheti cha usajili kitakacholipiwa ada ya kila mwaka.
- Umiliki wa cheti cha usajili hautahamishika isipokuwa kwa idhini ya Bodi
- Bodi inaweza kufuta usajili kabla ya muda wake kwisha, endapo mdau atashindwa kukidhi vigezo vya usajili.
- Endapo kutakuwa na mabadiliko ya anuani, maombi ya kubadilisha cheti yatumwe katika ofisi za Bodi ndani ya siku 45.
- Endapo cheti cha usajili kitapotea au kuharibika, mdau atoe taarifa kwa msajili wa Bodi kwa kuwasilisha ushahidi wa vielelezo vya upotevu kutoka polisi. Bodi ikiridhika na ushahidi itatoa nakala iliyoidhinishwa (*certified copy*) kwa gharama ya shilingi 10,000/=.

Faida za kujisajili

- Kutambulika na kuwa mdau halali wa tasnia ya nyama;
- Kutambulika kwa shughuli anazofanya na kushiriki katika mipango ya kuendeleza tasnia ya nyama;
- Kurahisisha upatikanaji wa soko la mifugo, nyama na bidhaa zake;
- Kurahisisha uratibu wa shughuli za kuendeleza tasnia ya nyama (uzalishaji wa mifugo, nyama na bidhaa zake);
- Kurahisisha ufuatiliaji wa ubora na usalama wa nyama na mazao yake kwa afya ya mlaji;
- Kuhakikisha upatikanaji wa mbinu na teknolojia sahihi za uzalishaji wa nyama bora;
- Kuwa na mawasiliano mazuri ya kibiashara kati ya wadau mbali mbali na kufahamu mahitaji ya soko na uwezo wa kuhudumia mahitaji hayo;
- Kuwa na mazingira mazuri ya ushindani wa haki kibiashara; na
- Kukubalika kwa bidhaa za mdau katika soko.

Hasara za kutosajili

- Kutotambulika kuwa mdau halali wa tasnia ya nyama; na
- Kuzuiwa kufanya biashara yoyote katika tasnia ya nyama ikiwa ni pamoja na kufuga mifugo ya nyama kwa ajili ya biashara, kutouza mifugo na nyama, kutoendesha shughuli za mnada, kutochinja, kutosindika na kutoendesha shughuli za vyama vya wadau.

Uhalali wa Cheti cha usajili

- Cheti cha usajili kitadumu kwa mwaka mmoja;
- Kitalipiwa ada ya kila mwaka ili kukitunza;
- Bodi inaweza kusitisha au kunyang'anya usajili kabla ya muda, endapo mdau atashindwa kukidhi masharti ya usajili na hivyo kupoteza sifa ya usajili.

Rufaa

- Mdau ambaye hataridhishwa na maamuzi ya Bodi ya kutomsajili, kufuta au kunyang'anywa usajili ana haki ya kukata rufaa kwa Waziri mwenye dhamana na Mifugo; na
- Rufaa kwa Waziri iambatanishwe na maamuzi ya Bodi aliyopewa ndani ya siku 30 tangu alipopokea maamuzi hayo.

Makosa na adhabu

- Mdau ambaye hatasajili au kwenda kinyume na maelekezo yaliyotolewa atakuwa amefanya kosa na atastahili adhabu ya faini au kifungo jela kulingana na hukumu ya mahakama. Endapo mdau atarudia kosa, adhabu kali zaidi itatolewa.

Kwa maelezo zaidi wasiliana na:
Bodi ya Nyama Tanzania
S.L.P 6085 DSM,
Regent Estate, Mtaa wa Ursino, Nyumba Na.13 Mikocheni
Simu:+255713412756
Barua pepe : info@tmb.go.tz